

Ni Nani Ninayeweza Kuwasiliana Naye kwa Usaidizi wa Elimu Maalum kwa Mtoto Wangu?

Kuna rasilimali za kukusaidia wewe na mtoto wako. Unaweza kujifunza kuhusu haki zako za kisheria na mahali pa kupata usaidizi. Usiogope kuomba usaidizi. Zifuatazo ni sehemu chache zinazoweza kukusaidia:

Idara ya Usalama wa Uchumi ya Arizona (Department of Economic Security, DES), Mpango wa Mikakati ya Mapema (Early Intervention Program, AzEIP)

(602) 532-9960

des.az.gov/services/disabilities/developmental-infant

Hutoa usaidizi na rasilimali kwa familia zenye watoto wachanga na wanaoenda dede walio na ulemavu chini ya miaka 3.

Arizona DES, Kitengo cha Ulemavu wa Ukuaji (Division of Developmental Disabilities)
1-(844) 770-9500
des.az.gov/services/disabilities/developmental-disabilities/

Hutoa huduma kwa watu wanaostahiki walio na ulemavu wa ukuaji na familia zao.

Idara ya Elimu na Huduma za Kipekee kwa Wanafunzi ya Arizona (Arizona Department of Education, Exceptional Student Services)

(602) 542-4013

azed.gov/specialeducation

Huhakikisha wanafunzi wote wa shule za umma wanaostahiki ambao wana ulemavu wanapewa elimu ya bila malipo na inayofaa.

Kuwalea Watoto Walio na Mahitaji Maalum (Raising Special Kids, RSK)
(602) 242-4366 au (800) 237-3007
Raisingspecialkids.org

Shirika lisilo la faida ambalo linatoa rasilimali na mafunzo kwa familia za watoto walio na ulemavu hadi umri wa miaka 26.

RSK pia inaweza kutoa usaidizi wa mchakato wa shule wa Mpango wa Elimu Iliyobinafsishwa (Individualized Education Program, IEP).

Kituo cha Sheria ya Ulemavu cha Arizona (Arizona Center for Disability Law, ACDL)

(602) 274-6287

azdisabilitylaw.org

Shirika lisilo la faida ambalo linaendeleza na kulinda haki za kisheria za uhuru, haki na usawa kwa watu walio na ulemavu. Maono yake ni jamii ambayo watu walio na ulemavu wanafurahia ukubalifu bila vizingiti.



Mpango wa Makao kwa Wakimbizi wa Arizona
1789 West Jefferson
Phoenix, Arizona 85007
Simu: (602) 542-6045

